MMUST PUBLISHING PRESS

Jarida la Kiswahili Sanifu

# Matumizi ya mkabala njia mseto katika ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili katika shule za upili

Kelvin Ihaji *, Frida Miruka, John K'Mraiji

*Idara ya Elimu ya Lugha na Fasihi, Shule ya Elimu, Chuo Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Masinde Muliro, Kakamega, Kenya*

**IKISIRI**

Maandalizi ya walimu huangazia vipengele mbalimbali ili kufaulisha ufundishaji unaofaa. Mojawapo ya vipengele hivi ni matumizi ya mkabala njia mseto katika ufundishaji ili kuimarisha uelewa wa wanafunzi. Licha ya hali hii, walimu wengi hupendelea kutumia mbinu moja ambayo hukuruza uelewa wa mada husika na hivyo kuathiri matokeo katika somo la Kiswahili. Lengo la makala hii ni kudadavua matumizi ya mkabala njia mseto katika ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili. Makala imejikita katika nadharia ya Mawasiliano iliyoasisiwa na Hodge & Kress (1988) na kuendelezwa na Kress (2010) na muundo wa usoroveya fafanuzi. Utafiti uliohusika ulilenga walimu na wanafunzi wa kidato cha tatu katika shule za upili za upeo za Kaunti ya Kakamega. Makala inaonyesha kuwa walimu wengi (80%) hutumia mkabala njia mseto katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili. Walimu wana ufahamu wa njia za mawasiliano na mbinu za kufundisha ila hawana ufahamu kuwa wanapotumia njia za mawasiliano na mbinu za kufundisha wanashirikisha mkabala njia mseto. Makala hii ilihitimisha kuwa matumizi ya mkabala njia mseto huongeza motisha, huvuta umakinifu na huhakikisha ufanisi katika somo la Kiswahili. Makala inapendekeza kuwa mkabala njia mseto utumike ili kuboresha ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili. Vilevile warsha, semina na symposia kuhusu mkabala njia mseto kwa walimu wa Kiswahili katika shule za upili ziandaliwe ili kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili kwa mkabala njia mseto.

**KUHUSU MAKALA**

*Maneno Muhimu:*
Mkabala njia mseto
Mbinu za kufundisha
Njia za mawasiliano
Uimarishaji
Ufundishaji wa Kiswahili

*Historia ya Makala:*
Tarehe ya Kutumwa: 25 Mei 2024
Tarehe ya Kurekebishwa: 23 Julai 2024
Tarehe ya Kukubalika: 10 Oktoba 2024
Mtandaoni: 27 Novemba 2024

## 1. Utangulizi

Ufundishaji na ujifunzaji hutegemea mawasiliano kwa ufanisi wake. Kwa hivyo, mwalimu anastahili kuzifahamu vyema njia za mawasiliano kama vile: mawasiliano ya kufasiri, mawasiliano ya uwasilishaji, mawasiliano ya kibinafsi na Mkabala Njia Mseto (MNM) ambayo huhusisha matumizi ya njia mbili au zaidi za mawasiliano kama vile kusikiliza, kuona, kusoma na kuandika na utendaji. Pia afahamu jinsi ya kutumia kila njia katika ufundishaji wa somo la Kiswahili. Ufahamu na matumizi ya MNM katika ufundishaji na ujifunzaji huleta ufanisi mkubwa wa kiakademia miongoni mwa wanafunzi na pia katika taaluma ya ualimu. Kress & Van (2006) wanaeleza kuwa MNM ni matumizi ya njia mbalimbali kuwasilisha ujumbe. Baadhi ya njia za mawasiliano walizotaja ni kama vile: matumizi ya picha, ishara, sauti zilizorekodiwa na kuzuru maeneo tofauti. Makala hii inatathmini matumizi ya njia walizotaja na zaidi katika ufundishaji wa Kiswahili ili kuonyesha kuwa ufundishaji na ujifunzaji ni mchakato wa mawasiliano.

Kama ilivyo katika usetaji wa mbinu za ufundishaji, ni muhimu kutumia mkabala njia mseto ili kufaidi sampuli mbalimbali za wanafunzi darasani. Usetaji wa njia za mawasiliano huhusisha njia za kusikiliza, kuona, kusoma na kuandika na utendaji. Mwalimu anastahili kufahamu jinsi ya kutumia kila njia katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili. Ufahamu na matumizi ya MNM katika ufundishaji na ujifunzaji, huleta ufanisi mkubwa wa kiakademia miongoni mwa wanafunzi na pia katika taaluma ya ualimu. Kwa mujibu wa Kothari (1992), ufundishaji mzuri ni ule unaoshirikisha njia tofauti, wala haulengi kupata ufanisi kwa kutumia mbinu moja tu. Mafunzo yanayotokana na mkabala njia mseto huhakikisha kuwa maana inapatikana kwa kutumia mkabala njia mseto, kwa mfano, bango hutoa maana kupitia maandishi ya lugha, picha na mitindo tofauti. Makala hii inatathmini matumizi ya mkabala njia mseto katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili.

* Mwandishi Mkuu. Simu: +254716270717; Barua Pepe: ihaji.kelvin@gmail.com
Mhariri: Leonard Chacha Mwita, Chuo Kikuu cha Kenyatta, Kenya.
Nukuu: Kelvin I., Frida M., & John K. (2024). Matumizi ya Mkabala njia mseto katika Ufundishaji na Ujifunzaji wa Kiswahili katika Shule za upili. Jarida la Kiswahili Sanifu 1 (2024), 1 – 7.

© 2024 Creative Commons Attribution License (CC BY-NC-SA).

### 1.1. Mkabala Njia Mseto

Wataalum wameiangazia dhana ya mkabala njia mseto kwa namna mbalimbali. Kress & Leeuwen (2002) wanasema kuwa mkabala njia mseto ni matumizi ya njia ya mawasiliano pamoja na mbinu ya kufundishia ili kuwasilisha ujumbe. Kwa mfano kwenye kitabu ambacho kina picha na maandishi, picha ni njia ya mawasiliano na kuandika ni mbinu moja ya kufundishia yote yakiwekwa pamoja yanawasilisha ujumbe faafu kwa wakati mmoja. Kulingana na maoni ya Kress & Leeuwen (2002), Bezemer & Mavers (2011) na Lutkewitte (2014) ni wazi kuwa MNM ni matumizi ya zaidi ya mbinu moja na njia ya mawasiliano ili kuwasilisha ujumbe unaokusudiwa.

Kress (2010) anasema kuwa kila njia huwa na kazi maalum katika kuwasilisha maana. Katika kitabu cha picha, maandishi na picha hueleza hadithi nzima ila kwa njia tofauti. Guijairo (2009) anasema kuwa picha hueleza kuhusu hadithi iliyoandikwa, pia hutumika kueleza mitazamo tofauti kuhusu hadithi na wakati mwingine hutofautiana na maneno yaliyoandikwa. Huu uwasilishaji wa ujumbe kupitia njia mbalimbali ndio msukumo unaotuelekeza kuchunguza matumizi ya mkabala njia mseto katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili. Walioandika kuhusu MNM kwa ubunifu walichanganya njia katika miktadha mbalimbali ili kuleta maana inayotarajiwa. Matumizi ya MNM darasani huibua ubunifu kwa mwalimu na mwanafunzi. Kalantzis & Cope (2020) wanasema kuwa MNM si matumizi ya teknolojia tu bali hushirikisha njia kama vile kusoma kwa kuona, kusoma kwa kisikiliza, kusoma kwa kuandika, kusoma makala na pia kuzuru maeneo mbalimbali kwa nia ya kusoma.

Kress (2005) akichunguza matumizi ya mkabala njia mseto katika ufundishaji wa lugha ya Kiingereza katika shule za upili Uingereza, anaangazia njia za mawasiliano drasani kama vile: matumizi ya picha, ishara, miondoko ya mwili, sauti zilizorekodiwa, maandishi, muziki na hotuba. Anasema kuwa matumizi ya mkabala njia mseto yanahusisha matumizi ya vifaa na mbinu mbalimbali na hurahisisha ujifunzaji. Maelezo haya ni ya jumla sana kuhusu mkabala njia mseto. Kuna haja ya kubainisha matumizi ya mkabala njia mseto katika ufundishaji na ujifunzaji.

### 1.2. Misingi ya Nadharia

Makala hii inaongozwa na nadharia ya mawasiliano njia mseto iliyoasisiwa na Hodge & Kress (1988) na kuendelezwa na Kress (2010). Hodge & Kress (1988) waliibua nadharia hii walipokuwa wanachangia mjadala uliokuwepo wa nafasi ya "picha" katika mawasiliano. Nadharia hii inafafanua nafasi ya picha katika mawasiliano. Aidha inafafanua kuwa uzuri wa kitu unategemea hali ya kuvutia inayochorwa na picha hiyo. Kwa mujibu wa Kress (2009), nadharia ya mawasiliano njia mseto ni aina ya nadharia inayoangazia mbinu nyingi na tofauti ambazo watu hutumia ili kujieleza na kuwasiliana na wenzao. Kress anaeleza kuwa nadharia hii ina ufaafu mkubwa kwa sasa baada ya ujio wa vifaa vya kiteknolojia ambavyo vimerahisisha mawasiliano miongoni mwa watu, njia za kimawasiliano zinazotokana na ujio huo ni sanaa, uandishi, uimbaji na kusakata densi na mwingiliano wa kila siku. Njia hizi hujihusisha sana na uchunguzi wa mawasiliano ya kijamii ili kuchunguza mbinu zinazotumika kuwasilisha ujumbe na namna zinavyovutia katika mawasiliano, yaani hisia zinazoibuliwa na mbinu hizo (Bowen & Whithaus, 2013).

Usetaji katika mawasiliano huhusisha mbinu kama rasilimali zinazojengwa na jamii na kukubalika kitamaduni na zinazotumika kubeba maana, kwa mfano picha, maandishi, mpangilio, muziki, ishara, hotuba, picha zinazotembezwa na sauti zinazotolewa na vifaa mbalimbali (Kress, 2010). Mbinu hizi ni sehemu ndogo ya maana katika mawasiliano na hata huzifananisha na mofimu katika isimu, kwa hivyo kulingana naye mbinu huwa na athari kubwa katika uwasilishaji wa ujumbe. Hivyo basi makala inaongozwa na mihimili mitatu ya MNM ya rasilimali za kisemiotiki ambazo ni ishara (Hodge & Kress, 1988); matumizi ya mbinu anuwai zinazovutia katika mawasilaino (Kress, 2009); na athari za mbinu za mawasilaino katika ujumbe (Kress, 2010).

## 2. Uhakiki wa Maandishi

Wataalum mbalimbali kama vile Kress (2001), Jewitt (2006) na Kress & Leeuwen (2006) waliangazia MNM kwa njia tofauti zilizofaa kazi yetu. Kress (2001) aliangazia matumizi ya MNM katika ufundishaji na ujifunzaji huku uchunguzi wake ukishughulikia namna ya kuwasiliana katika darasa la somo la sayansi. Kutokana na utafiti wao walibaini kuwa kila njia ya mawasiliano ya ufundishaji huwa na jukumu lake mahsusi katika kuwasilisha ujumbe katika somo la sayansi na kwa hivyo walimu wanafaa kutumia MNM ili kuhakikisha kuwa wanafunzi wengi wameelewa somo. Utafiti wa Kress (2001) unajenga kazi yetu kwa kutoa maelezo kuhusu MNM ila unatofautiana na utafiti wetu kwani waliangazia matumizi ya MNM katika somo la sayansi huku utafiti wetu utaangazia mkabala njia mseto katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili.


Jewitt (2006), akichunguza mawasiliano darasani, alieleza kuwa si vifaa vya kiteknojia tu vinavyotumika kuwasiliana darasani kupitia kwa MNM bali vifaa vingine vya kisemiotiki ambavyo hufanya ufundishaji na ujifunzaji kuwa bora. Utafiti wake Jewitt ulikuwa muhimu kwa kazi yetu kwani ulichunguza mawasiliano darasani kwa ujumla. Makala hii inazama zaidi katika kuangazia MNM darasani wakati wa somo la Kiswahili. Kress & Leeuwen (2006) walipochunguza lugha na mawasiliano kwa kuangazia njia ya kutazama, walibaini kuwa kwa kutumia njia hiyo moja kuna vipengele muhimu ambavyo havifundishwi katika taasisi ya elimu. Kazi ya Kress na Leeuwen ilituelekeza kuchunguza njia zaidi zinazoweza kutumiwa katika sekta ya elimu ili vipengele vyote vya somo husika vifundishwe. Makala hii inaanagazia somo la Kiswahili na kuchunguza namna mkabala njia mseto unavyoweza kuhakikisha kuwa vipengele vyote vimefundishwa.

## 3. Njia na Mbinu za Utafiti

Sehemu hii inaangazia njia na mbinu za utafiti. Inashughulikia muundo wa utafiti na vipengele vyake kama ukusanyaji data, uchanganuzi na uwasilishaji wa data.Makala hii inarejelea muundo wa kithamano. Kutokana na mkabala huu, makala inahusisha muundo wa

usoroveya fafanuzi. Makala inatumia mseto wa sampuli za kimatilaba, kitabakishi na kinasibu. Kulingana na Simiyu (2022), usampulishaji wa matilaba ni mbinu ambayo humpa mtafiti uhuru wa kuteua kimaksudi sampuli anayotaka kwa ajili ya kukidhi malengo ya utafiti wake. Sampuli hii ilimsaidia mtafiti kuchagua shule za upeo za kaunti katika kaunti ndogo za Shinyalu, Ikolomani na Lurambi pamoja na wanafunzi na walimu wa Kiswahili walioshirikishwa. Kwa utabakishi, mtafiti aligawanya shule katika makundi kama vile: shule za wavulana za bweni (SVB), shule za wasichana za bweni (SSB) na shule mseto ya bweni (SMB). Kupitia kwa mbinu ya kinasibu watafitiwa walichaguliwa kutoka kwa orodha au kundi la nambari au majina. Mbinu hii ilitumika zaidi ikizingatiwa kuwa kidato cha tatu katika shule hizo kina mikondo miwili au zaidi.

Eneo la utafiti lilikuwa aunti ndogo za Shinyalu, Ikolomani na Lurambi katika Kaunti ya Kakamega. Utafiti ulilenga walimu na wanafunzi katika shule ishirini na sita (26) za upeo za kaunti katika eneo la utafiti. Kwa mujibu wa Adlam na wenzake (2011) kundi lengwa ni jumla ya vitu vyote vinavyohusika katika utafiti. Data asilia ilikusanywa kutoka kwa walimu na wanafunzi wa kidato cha tatu katika shule za upili za upeo za kaunti ya Kakamega. Njia na vifaa vya ukusanyaji data vilikuwa usaili, mahojiano, hojaji na orodha ya uchunzaji mtawalia (Kothari,1990; Dawson, 2002). Walimu10 kati ya 30 walihojiwa huku 20 wakipewa hojaji. Kwa upande mwingine anafunzi wote katika mikondo iliyoteuliwa walihusika katika uchunzaji.




Tak. 1: Mbinu na njia za mawasiliano za kuona

Data kutoka kwa hojaji hizi ilipangwa katika dhamira na kuwasilishwa kwa unukuzi wa semi mbalimbali. Hii data ilisaidia kueleza waziwazi majibu ya washiriki katika maswali funge. Katika utafiti huu, data kutoka maswali wazi ililinganishwa miongoni mwa watafitiwa, iliainishwa na mwishowe kufariwa. Maelezo yaliyohusiana na data ya kitakwimu yalikusanywa katika hojaji za maswali funge na kuripotiwa kidondoo na hivyo kuweka wazi matokeo. Mahojiano yalitekelezwa kwa walimu na orodha ya uchunzaji ikatumiwa kukusanya data darasani kwa kutazama na kunukuu mbinu na MNM alizotumia mwalimu katika ufundishaji. Uchanganuzi ulihusisha kuweka data katika misimbo, kupangwa na kuchanganuliwa kwa kutumia mbinu ya kithamano. Hatua ya kwanza katika uchanganuzi wa data ya kithamano ilikuwa kusikiliza semi zote za mahojiano za kundi lengwa zaidi ya mara moja kisha kunakili simulizi zote kwa kipakatalishi. Baada ya kunakili kwa kipakatalishi, dondoo zilichukuliwa na kupitiwa na mtafiti kisha zikachanganuliwa kulingana na madhumuni ya utafiti. Data ya kitakwimu ilichanganuliwa na kuwasilishwa katika majedwali kwa asilimia. Maswali ambayo Mathews & Ross (2021) wanazua yalikuwa mwongozo muhimu katika kupanga na kuichanganua data. Mathalani: Ni data gani muhimu? Ni data gani inayofanana? Vitengo gani vitatumika kuwasilisha data?

## 4. Matokeo na Majadiliano

### 4.1. Matumizi ya MNM katika Ufundishaji wa Kiswahili

Makala hii inatalii namna MNM hutumika katika ufundishaji wa Kiswahili katika shule za upili. Inaonyesha jinsi mbinu za ufundishaji hutumika pamoja na njia za mawasiliano za kuona, kusikiliza, kusoma, kuandika na utendaji.

#### *4.1.1. Ishara*

Matokeo haya yanaonyesha kuwa walimu 30 ambao ni 100% walikiri kutumia ishara kama njia moja ya mawasiliano wakati wa kufundisha somo la Kiswahili. Walimu waliotumia ishara kama njia moja ya kuwasiliana walikiri kuwa ishara hutumika pasipo kupangwa, kwamba mwalimu hujipata akieleza suala kwa kutumia ishara kama anavyoeleza Cooper, (2002). Kwa mfano, katika shule ya wasichana ya B, mwalimu aliwaelekeza wanafunzi kwenda kwenye makundi ya wanafunzi kumi kwa kutumia ikono kuashiria "kuja pamoja kwa wanafunzi kumi katika kundi moja". ia alitumia kidole kilichogusa mdomo kuashiria kuwa kulikuwa na kelele kwa hivyo anataka utulivu. Baada ya ishara hiyo darasa lilikuwa kimya akaendelea kupeana miongozo katika makundi. Matokeo haya yanalingana na maoni ya Seyedeh na wenzake (2011), wanaosema kuwa wanafunzi hujifunza kwa kuona. Wanaojifunza kutokana na njia hii hupendelea matumizi ya njia za mawasiliano kama vile matumizi ya ishara, picha, projekta, ramani, majedwali na chati. Picha, kwa mujibu wa Hodge & Kress (1988), huonyesha uzuri wa kitu ambao hutegemea hali ya kuvutia inayochorwa na picha hiyo.

#### *4.1.2. Picha Mjadala na Kuandika*

Kwa upande mwingine, walimu ishirini na saba (27) ambao ni 90% kati ya thelathini (30) ambao ni 100% walioshiriki katika utafiti huu walikiri kutumia njia ya picha, mijadala na kuandika kudhihirisha MNM darasani. Picha ni nyenzo muhimu ya ufunzaji kama wanavyoeleza Oktaviani & Mandasari (2020) kuwa matumizi ya nyenzo katika ufundishaji huboresha motisha ya wanafunzi kutaka kujifunza somo husika. Katika Shule ya Wavulana E, mada ya ufundishaji wa sauti ilitangulizwa na majadiliano na kisha kutumia mchoro wa sehemu za kutamkia uliowafanya wanafunzi kutaka kujua zaidi kuhusu sauti zinazotumika katika ala zilizoonyeshwa kwenye mchoro na baadaye wanafunzi waliweza kuandika na hata kuchora kielelezo vitabuni ili kujisomea baadaye. Kwa mujibu wa Wright & Haleem (2001), picha


huwachochea wanafunzi kutaka kujua zaidi kuhusu kilicho kwenye picha na kuandika huwafanya kukumbuka walichosoma. Picha kama rasilimali ya kisemiotiki ina dhima kuu katika nadharia ya MNM (Hodge & Kress, 1988).

#### 4.1.3. Usetaji wa Projekta, Mhadhara na Kuandika

Usetaji mwingine ulihusisha matumizi ya Projekta, mhadhara na kuandika. Matumizi ya projekta yanahusisha kuona kwa maandishi yanayomulikwa na projekta.Kati ya walimu (30) waliohusishwa kwenye utafiti huu, walimu (10) ambao ni asilimia (33%) walitumia projekta, mhadhara na kuandika na hivyo kudhihirisha MNM. Hii ni idadi ndogo ikilinganishwa na idadi ya walimu katika Kaunti ya Kakamega. Hali hii inashadidiwa na Amin na wenzake (2018) wanaosema kuwa ingawa njia hizi zinatumiwa, baadhi ya walimu huzipuuza. Wanaongeza kuwa matumizi ya projekta kwenye vipindi vya mhadhara na kuandika katika ufundishaji wa somo la Kiswahli hufanya darasa liwe mahali pazuri pa kusomea na kuwasiliana. Makala hii inahimiza kushirikishwa kwa vifaa vya kiteknolojia katika ufundishaji wa Kiswahili. Coppola & Thomas (2001) wanashikilia kuwa matumizi ya vifaa vya kiteknolojia kama vile projekta katika kipindi huwafanya wanafunzi kushiriki sana na vilevile huongeza motisha yao. Kwa mujibu wa Kress (2009) nadharia ya MNM ina ufaafu mkubwa kwa sasa baada ya ujio wa vifaa vya kiteknolojia ambavyo vimerahisisha mawasiliano.

### 4.2. Kusikiliza

Kitengo hiki cha usetaji kilihusisha kusikiliza na kuzungumza. Utafiti ulionyesha kuwa njia mbalimbali za mawasiliano hutegemea usikivu ili kujifunza. Matokeo yamewasilishwa katika Tak. 2.




Tak. 2: Njia za mawasiliano za kusikiliza

#### 4.2.1. Usetaji wa Redio, Makundi na Mhadhara

Matokeo katika Tak. 2 yanaonyesha kuwa walimu 20 (asilimia 66) kati ya 30 walikiri kutumia usetaji wa redio, makundi na mhadhara katika ufundishaji wa somo la Kiswahili. Katika shule ya wavulana G, mkuu wa somo la Kiswahili alitaja kuwa walimu katika idara ya Kiswahili hutumia njia mbalimbali za kuwasiliana na wanafunzi darasani redio ikiwa moja yao. Aliendelea kueleza kuwa redio huwasaidia wanafunzi kuelewa mambo kwa urahisi na pia husaidia wanafunzi walio na matatizo ya matamshi kuwa bora kwa sababu wanafunzi huwa na nafasi ya kurudia matamshi baada ya kutamkwa katika redio wakiwa kwenye makundi. Fleming & Baurne (2006) wanashadidia suala hili kwa kusema kuwa wanafunzi wanaojifunza kwa njia ya kusikiliza kwa makini huwa na sifa kama vile kukumbuka kwa urahisi ujumbe uliosemwa. Mkuu wa somo alitaja mfano wa vipindi vya ushairi ambavyo walimu wa Kiswahili katika kidato cha tatu hufundisha kwa mhadhara wakitumia redio ili wanafunzi waweze kuimba au kukariri mashairi kwa njia inayofaa. Maoni ya mwalimu yanashadidiwa na Odera (2011) ambaye alibaini kuwa matumizi ya redio husaidia wanafunzi kukumbuka misamiati na utamkaji. Utafiti huu uligundua kuwa walimu huseta matumizi ya redio kama njia ya mawasiliano na mbinu za makundi na mhadhara ili kufaulisha kipindi. Kress (2010) katika nadharia ya MNM anashadidia kuwa matumizi ya mbinu anuai ni muhimu ili kufaulisha mchakato mzima za mawasiliano.

#### 4.2.2. Usetaji wa Rununu, mhadhara na makundi

Matokeo yanabaini kuwa walimu 25 kati ya 30 ambao ni asilimia 83 waliseta rununu, mbinu ya mhadhara na makundi ili kukidhi mahitaji ya kipindi cha somo la Kiswahili. Kwa mfano, katika shule ya wavulana C, mwalimu alieleza kuwa wanafunzi wanapokuwa kwenye makundi yeye hukagua kila kundi na kuwaongoza kutumia mifano kutoka kwenye rununu wanapojadiliana na kukosa mifano zaidi .Ikilinganishwa na usetaji wa njia zingine za mawasiliano, matumizi ya rununu na mbinu zingine za ufundishaji zilisheheni mno kwa sababu ya ukuaji wa teknolojia.Walimu katika eneo husika walipendelea matumizi ya rununu kuliko ya redio kwa madai kuwa ilikuwa njia ya kale ya mawasiliano. Hali hii inashadidiwa na Kukulska-Hulme (2009). Kwa mujibu wa Matimbwa & Anney (2016), mawasiliano ya kiteknolojia ni suala ambalo halijaacha ufundishaji na ufunzaji.


#### 4.2.3. Usetaji wa Ufunzaji wa Moja kwa Moja, Mhadhara na Majadiliano

Matokeo yanaonyesha kuwa walimu 27 kati ya 30 ambao ni asilimia 90, walitumia au walikiri kutumia ufunzaji wa moja kwa moja pamoja na mbinu za mhadhara na majadiliano ili kufaulisha kipindi chao. Njia hii ya mawasiliano darasani katika kundi la kusikiliza ilitumika sana ikilinganishwa na njia zingine za mawasiliano darasani. Walimu wa somo la Kiswahili katika shule zote tulizozuru walikubali kuwa wanapofundisha kwa mhadhara wao huwasiliana na wanafunzi huku wakisikiliza kwa makini kwenye makundi yao. Walimu walitaja kuwa wanapowasiliana na wanafunzi darasani huwa kuna utaratibu na kila mmoja huwa na nafasi yake ya kuzungumza, kwa hivyo ujumbe hufika bila tatizo. Hata hivyo, Drago & Wagner (2004) wanadokeza kuwa anafunzi wanaojifunza kwa kusikiliza wanaweza kukatiziwa masomo iwapo kutakuwa na kelele.

#### 4.2.4. Usetaji wa Mawasilisho darasani, Makundi na Mhadhara

Mtafiti alibaini kuwa walimu 20 kati ya 30, mbao ni silimia 67, alitumia usetaji wa mawasilisho darasani,

mbinu ya makundi na mhadhara katika ufundishaji wa somo la Kiswahili. Walimu wanaofundisha somo la Kiswahili katika shule za upili tulizozuru walikiri kuwa wao huwasiliana na wanafunzi wakati ambapo wanawasilisha kazi walizopewa kwenye makundi yao. Katika uwasilishaji huo kuna viongozi wanaowasilisha na wengine kusikiza kwa makini, baadaye mwalimu huhitimisha mawasilisho yote kwa kutoa mhadhara kuhusu somo au mada iliyozungumziwa. Caruso na wenzake (2017) wanashadidia matokeo haya wanaposema kuwa kusikiliza ni njia mojawapo ya kuwasiliana ambayo haiwezi kuepukika. Makosa mengi zaidi ya asilimia 60 hutokea kwa sababu ya kutoelewa kunakotokana na usikilivu mbaya.



**Tek. 3**: Njia za mawasiliano za kusikiliza

### *4.2.5. Usetaji wa Kusoma na kuandika na Mbinu za kufundisha*

Walimu 28 kati ya 30, ambao ni asilimia 93, waliseta njia ya kusoma na kuandika pamoja na mbinu za kufundisha. Kupitia kwa njia hii ya mawasiliano, wanafunzi wa somo la Kiswahili hujifunza kwa njia ya kuandika na kusoma. Kwa mfano, katika shule ya wavulana ya B kupitia ufunzaji darasani tulibaini kuwa wanafunzi wakiwa kwenye makundi, mwalimu aliwateuwa wanafunzi kusoma vifungu vya ufahamu huku wengine wakisikiliza na kufuatilia kwa makini. Katika mawasiliano ni sharti upande mmoja uwe umetulia wakati upande mwingine unawasilisha ujumbe. Njia hii ya kusoma kwa sauti kifungu au aya ilijitokeza wazi na ili kufahamu kuwa ujumbe na vifungu walivyokuwa wakisoma darasani vimeeleweka, mwalimu aliuliza maswali mwisho wa somo; mikono iliyonyoshwa ili kujibu na michango iliyotolewa na wanafunzi iliashiria kuwa somo lilieleweka.

Kwa mujibu wa Fleming & Mills (1992), ujumbe katika njia ya kusoma darasani huwasilishwa kwa maandishi. Wanafunzi waliojifunza kwa njia hii ya mawasiliano walisoma kwa vitabu, mwalimu kuandika ubaoni, wanafunzi kuandika maelezo marefu, kuandika maelezo ya kufafanua picha, kujibu maswali kwenye vitabu vyao na kusoma kwa sauti vifungu. Walimu na wakuu katika somo la Kiswahili katika shule tulizozuru walitaja hiki kikao kama njia ya pekee inayotumika na kila mmoja kufundisha Kiswahili. Uchunzaji wa darasani pia ulithibitisha matumizi ya kusoma na kuandika na mbinu nyingine za kufundisha.

## 4.3. Utendaji

Utendaji ulijitokeza kama njia mojawapo inayotumika pamoja na mbinu nyingine za mawasiloano. Utafiti ulibaini usetaji wa mbinu za utendaji kwa namna mbili: Tak. 3, linaonyesha matokeo haya.

i. Usetaji unaohusu maonyesho, makundi na mhadhara.
ii. Usetaji unaohusu ziara, makundi na maswali na majibu.

### *4.3.1. Usetaji wa Maonyesho, Makundi na Mhadhara*

Matokeo katika Tek. 3 yanaonyesha kuwa walimu 25 kati ya 30 (asilimia, 83) waliseta maonyesho, makundi na mhadhara ili kufaulisha somo la Kiswahili. Njia hii ilitumika sana katika kundi hili la utendaji kwa sababu kuzuru maeneo mbalimbali kama njia ya mawasiliano katika somo la Kiswahili hakukuruhusiwa kwa sababu ya kuhofia msambao wa virusi vya korona. Katika shule ya mseto ya D, katika uchunzaji, mwalimu alikuwa akifundisha kwa mbinu ya mhadhara kuhusu sauti na alipofikia sauti /p/ na /b/ aliwaeleza wanafunzi kutamka darasani ili kutofautisha sauti hizo. Katika hali hii utendaji ulisetwa na mhadhara. Utendaji huu ni njia ya mawasiliano pale ambapo mwanafunzi anatamka mwenyewe na kuelewa tofauti iliyoko kati ya sauti hizo.

Kwa upande mwingine usetaji unaohusu ziara, makundi na maswali na majibu ulitumiwa na walimu 18 kati ya 30 ambayo ni asilimia 60. Hii ni njia moja ya mawasiliano chini ya utendaji ila walimu wote walisema kuwa walikabiliwa na changamoto kutokana na fedha zinazohitajika kuzuru maeneo mbalimbali katika makundi ili kusoma kuhusu sajili za maeneo hayo. Vilevile katika kipindi cha utafiti kilichokuwa cha Korona mwaka wa 2021, serikali kupitia Wizara ya Elimu haikukubali wanafunzi kuzuru maeneo ambako wangetangamana na watu wengi wakihofia msambao wa korona shuleni. Mbali na ugonjwa wa Korona, changamoto nyingine ilikuwa ufadhili kwani ziara huhitaji fedha. Matokeo yalionyesha kuwa njia mbalimbali za mawasiliano husetwa na mbinu za kufundisha somo la Kiswahili ili kuhakikisha kuwa umakinifu wa wanafunzi umevutwa na mada husika imeeleweka vizuri na wanafunzi. Kress (2010) anashadidia kuwa MNM ina athari chanya kwa ujumbe na huimarisha uelewa katika miktadha anuwai. Kilichojitokeza wazi ni kuwa mbinu haiwezi ikatumika bila ya njia ya mawasiliano, kwa hivyo hata mwalimu asipojiandaa kwa kuseta njia ya mawasiliano na mbinu, vyote viwili hujitokeza tu katika kipindi. Matokeo yalionyesha kuwa walimu walitumia njia za mawasiliano za kuona, kusikiliza, kusoma na kuandika na utendaji pamoja na mbinu mbalimbali za kufundishia somo la Kiswahili kama ilivyodhihirika katika **Tak. 1**, **Tak. 2** na Tek. 3. Makala hii inaonyesha kuwa MNM hutumika katika ufundishaji wa Kiswahili kwa kuhusisha mbinu mbalimbali.

## 5. Hitimisho na Mapendekezo

### 5.1. Hitimisho

i. Makala hii inahitimisha kuwa MNM hutumika katika ufundishaji wa Kiswahili au kwa kupangwa au kutopangwa.
ii. MNM hutumika pamoja na mbinu za ufundishaji katika ufundishaji wa somo la Kiswahili. Mbinu zinazoongoza zinahusisha kuona (100%), pcha (90%), mwasiliano ya moja kwa moja (90%) na ksoma na kuandika (93%). Mbinu za kielektronika kwa upande mwingine hutumika kwa nadra. Kwa mfano pojecta (33%).
iii. Usetaji unaohusisha mbinu za kusikiliza ulitumika kwa wastani kwa 60% kwa redio, makundi na mhadhara.
iv. Usetaji wa stadi za mawasiliano za kusikiliza na kuongea, kusoma na kuandika na mbinu za ufundishaji ni kipengele muhimu katika kuimarisha ufunzaji wa Kiswahili.
v. Usetaji unaohusisha vifaa vya kielektroniki ni mchache licha ya kuwa vina ufaafu mkubwa katika ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili.

### 5.2. Mapendekezo

i. Utafiti unapendekeza kuwa MNM ihusishwe kama mbinu mojawapo ya kuhusishwa katika sera ya ufundishaji wa Kiswahili. Hali hii itawezesha walimu kupanga matumizi yake.
ii. Matumizi ya MNM yaimarishe matumizi ya vifaa vya kidijitali ili kuboresha ufunzaji katika enzi hizi za kidijitali
iii. Usetaji ujumuishe stadi zote za lugha kwa kuegemea stadi inayokuzwa katika somo husika mathalan, kusikikiza na kuongea, kusoma au kuandika.
iv. Warsha, semina na symposia kuhusu mkabala njia mseto kwa walimu wa Kiswahili katika shule za upili ziandaliwe ili kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili kwa mkabala njia mseto.

## Marejeleo


Adlam, S. B., Perera, S., Lake, R. J., Campbell, D. M., Williman, J. A., & Baker, M. G. (2011). Acute gastrointestinal illness in New Zealand: a community study. *Epidemiology & Infection*, *139*(2), 302-308.

Amin, M. R., Azim, M., & Kalam, M. A. (2018). The benefit of using multimedia projector in English Language teaching classroom. International Journal of Social Sciences & Humanities, 3(1), 62-76.

Bowen, T. &. Whithaus, (2013). Multimodal Literacies and Emerging Genres. Pittsburgh: University of Pittsburg Press.

Bezemer, J., & Mavers, D. (2011). Multimodal transcription as academic practice: A social semiotic perspective. International Journal of Social Research Methodology, 14(3), 191-206.

Caruso, M., Gadd Colombi, A., & Tebbit, S. (2017). Teaching how to listen. Blended learning for the development and assessment of listening skills in a second language. Journal of University Teaching & Learning Practice, 14(1), 14.

Cooper, M. L. (2002). Alcohol use and risky sexual behavior among college students and youth: evaluating the evidence. Journal of Studies on Alcohol, supplement, (14), 101-117.

Coppola, J. F., Thomas, B. A., & Thomas, J. D. (2001). The Effect of Technology Integration on Critical Thinking Skills in a Graduate Introductory Information Systems Course. In *Proceedings of the Information Systems Education Conference (ISECON)* (Vol. 18).

Dawson, C. (2002). Practical research methods: A user-friendly guide to mastering research.

Drago, W. A., & Wagner, R. J. (2004). Vark preferred learning styles and online education. Management Research News, 27(7), 1-13.

Fleming, N. D., & Mills, C. (1992). Not another inventory, rather a catalyst for reflection. To improve the academy, 11(1), 137-155.

Fleming, N., & Baume, D. (2006). Learning Styles Again: VARKing up the right tree! Educational developments, 7(4), 4.

Guijarro,A.J.(2019). Communicative functions of visual metonymies in picture books targeted at children in two different age groups. A multimodal analysis.Word, 65(4), 193 -212

Hodge, R. I. V., & Kress, G. R. (1988). Social semiotics. Cornell University Press.

Jewitt, C. (2006). Technology, Literacy and Learning: A Multimodal Approach. London: Routledge, Taylor and Francis Group.

Kalantzis, M., & Cope, B. (2020). After the COVID-19 crisis: Why higher education may (and perhaps should) never be the same. Educational Philosophy and Theory, 40(1), 51-55.

Kothari, C. R. (1990). Methodology, Methods and Techniques. New Delhi: Wiley Enstern Ltd.

Kothari, C. R. (1992). Methods and Techniques of Teaching. Sterling Publishers Pvt Ltd.

Kress, G. (2001). From Saussure to critical sociolinguistics: The turn towards a social view of language. Discourse theory and practice: A reader, 29-38.

Kress, G., & Van Leeuwen, T. (2002). Colour as a semiotic mode: notes for a grammar of colour. *Visual communication*, *1*(3), 343-368.

Kress, G. and T. van Leeuwen (2006). Reading Images: The Grammar of Visual Design, 2nd edn. London: Routledge.

Kress, G. (2009). Multimodality: A Social Semiotic Approach to Contemporary Communication. London: Routledge.

Kress, G. (2010). Multimodality. A Social Semiotic Approach to Communication. London: Routledge.

Kress, G. (2005). Introducing Social Semiotics. London: Routledge.

Kukulska-Hulme, A. (2009). Will mobile learning change language learning? ReCALL, 21(2), 157-165.

Lutkewitte, C. (2014). Multimodal composition: A critical sourcebook. Bedford/St. Martin's.

Mathews, J., & Ross, S. F. (2021). Proportionality Review in Pennsylvania Courts.

Matimbwa, R., & Anney, V. N. (2016). Teachers' and students' perceptions of self-driven acceptance of mobile phone use as an ICT teaching tool. Journal of Emerging Trends in Educational Research and Policy Studies, 7(2), 91-106.

Oktaviani, L., Mandasari, B., & Maharani, R. A. (2020). Implementing Powtoon to improve students'international culture understanding in English class. Journal of Research on Language Education, 1(1).

Odera, F. Y. (2011). Learning English Language by Radio in Primary Schools in Kenya. Online Submission.

Seyedeh Kolsoum, H. T., & Abbas, Z. (2011). Quality of Vocational Training in PHP and Sari. Australian Journal of Basic and Applied Sciences, 5(12), 3338-3342.

Simiyu, B. W. (2022). *Gaps in Informed Consent Process Among Women Who Have Undergone Elective Caesarean Section at AIC Kijabe Hospital, Kiambu County Kenya* (Doctoral dissertation).

Wright A., & Haleem S. (2001). Visuals for the Language Classroom. London and New York: Longman.